**HOTUBA YA MHESHIMIWA MWENYEKITI WA BARAZA LA BIASHARA LA MKOA WA KIGOMA MHESHIMIWA BRIG. GEN. (MST.) EMMANUEL MAGANGA KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA BARAZA TAREHE: 24 AGOSTI 2018 .**

**UKUMBI: OFISI YA MKUU WA MKOA KIGOMA.**

Mheshimiwa Katibu Tawala wa Mkoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wote Mkoani Kigoma,

Wakurugenzi wa Halmashauri, Manispaa na Halmashauri za Miji,

Mwenyekiti wa TCCIA - Mkoa,

Wageni waalikwa, mabibi na Mabwana,

Itifaki Imezingatiwa,

Habari za asubuhi.

Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha na kuwashukuru kwa kuitikia wito wa mkutano huu muhimu wa Baraza la Biashara la MKoa kwa mustakabali wa maendeleo ya Mkoa wetu Kiuchumi na Kijamii.

Ninatambua kuwa hiki ni kikao chetu cha kwanza kwa mwaka huu 2018 cha Baraza la Biashara la Mkoa wa Kigoma na nichukue fursa hii kuwashukuru waandaaji wote, Sekretarieti ya Baraza pamoja na Kamati Tendaji ya Baraza hili kwa juhudi kubwa kufanikisha mkutano huu. Pia naomba, kwa dhati kabisa kushukuru Mradi wa LIC kwa kuwezesha kufanyika kwa mkutano huu.

**Ndugu washiriki**

Napenda kuchukua nafasi hii kuwatambulisha kwenu viongozi wapya ambao hatukuwa nao katika Baraza la tarehe 23.11.2017, na sasa leo wanashiriki Baraza hili kwa mara ya kwanza. Namtambulisha kweny Katibu wa Baraza hili ambaye ni Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) anashiriki kwa mara ya kwanza baada ya kuhamishiwa mkoani Kigoma.

Namtambulisha Mkuu wa Wilaya ya Kasulu (atasimama) na Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe (atasimama). Naomba pia niwatambulishe Wakurugenzi wa Halmashauri ambao pia wamehamia Mkoani Kigoma. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Kakonko, Kigoma DC na Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Kwa pamoja, tunaungana sote katika kuendeleza juhudi za kuleta maendeleo katika mkoa wa Kigoma sambamba na ajenda ya Serikali ya kuwa na Uchumi wa Viwanda.

**Ndugu washiriki**

Wote tunaelewa kuwa mabaraza haya yana uwezo mkubwa wa kutatua changamoto za kibiashara na kuhimiza uwekezaji. Ninafahamu kuwa leo wote mmejipanga kikamilifu kuitumia siku hii kukamilisha mambo mliyoazimia kipindi kilichopita, kuangalia na kujipima namna ambavyo utekelezaji wa maazimio ya baraza la mwisho lilofanyika tarehe 23.11. 2017 ambayo ni Dira ya kuonyesha umuhimu wa uwepo wa mabaraza haya.

Pia nina taarifa kwamba wawakilishi wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) wako hapa kufuatilia ufanisi wa mabaraza haya. Aidha taasisi ya Sekta Binafsi Taifa (TPSF) nayo imewakilishwa ili kuungana na kuiinua Sekta Binafsi.

**Ndugu washiriki, mabibi na mabwana,**

Pamoja na hao, tunao wageni waalikwa ambao tunaweza kusema ni Taasisi alikwa, watakaotoa uelewa zaidi katika mada mbalimbali ambazo

zilijadiliwa katika baraza lililopita na zikaonekana ni changamoto na pia kuchangia katika mada zitakazowasilishwa leo.

Ikumbukwe kuwa mabaraza haya ya biashara yapo kwa mujibu wa sheria kutokana na Waraka wa Mheshimiwa Rais Na 1 wa Mwaka 2001 na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali Na 691 la tarehe 28 September 2001.

**Ndugu washiriki,**

Nina fahamu kuwa LIC kwa kushirikiana na TPSF Wamewajengea uwezo Sekta binafsi namna ya kuibua hoja na kutetea hoja husika kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa pamoja. Hivyo ninaamini kwa kutumia ujuzi mlioupata, tutakuwa na baraza zuri kabisa. Wote tuliopo hapa leo fursa tunazijua na tunaziona, ni wakati muafaka kuleta mapinduzi ya kiuchumi kwa kuhimiza uwekezaji katika viwanda. Kumbukeni kuwa Serikali ya awamu ya tano imeweka lengo la kuifanya Tanzania yetu kujenga uchumi wa Viwanda.

Wakati umefika sasa tuangalie jinsi ya kubadilisha uchumi wetu kwa kutumia viwanda hasa vile vya kusindika mazao yetu. Tuanzishe viwanda kulingana na rasilimali zilizopo ili tuzalishe bidhaa mbalimbali kwa gharama ndogo, kuziongezea thamani bidhaa na hivyo kuongeza pato kwa mfanyabiashara na Mjasiriamali. Washiriki tuelewe kuwa biashara ni kuthubutu, na sisi tufanye hivyo. Baadaye tutawasikia Wakurugenzi wa Halmashauri wakitoa wasilisho kutoka kila Halmashauri kuhusu namna wanavyoendeleza lengo la kuwa na viwanda na pia kutenga maeneo ya viwanda kwa mujibu wa maagizo na maelekezo waliyopewa na Serikali kuu.

Kigoma imekaa vizuri sana kibiashara hasa kwa kuangalia soko la ndani na soko lililopo kwa majirani zetu kama Burundi, DRC Congo, Zambia, Rwanda, Uganda na hata Sudan ya Kusini. Masoko haya ni fursa kwetu kuinua uchumi wetu kwa hiyo tuangalie ni bidhaa gani zinahitajika huko na tufanye kila jitihada kuyafikia masoko hayo kwa kuuza bidhaa

zilizoongezwa thamani na sio tena malighafi kama walivyofanya mabibi na mababu zetu.

**Ndugu washiriki,**

Nisisitize kuwa uaminifu ndio mojawapo ya misingi ya biashara endelevu. Hivyo ni vyema tujenge msingi huu vizuri kwa kuwa nimepata taarifa kuwa tumeanza kulaumiwa na wafanyabiashara wan chi jirani kuwa tumekuwa si waaminifu hasa tunapofanya biashara kwa kushirikiana na wafanyabiashara hao. Msingi mwingine ni kuwa na bidhaa bora na bei inayolingana na thamani ya bidhaa husika. Ninaelewa kuwa baraza hili sio la kukabiliana na changamoto tu bali pia kuibua mikakati na mipango ya kuinua uchumi wetu hapa mkoani. Ninaamini kama ilivyo ada, baraza hili litatoka na maazimio ambayo tutaweza kuyatekeleza na mapendekezo ya hatua zitakazochukuliwa kwa yale ambayo tutaona yako juu ya uwezo wetu.

**Hitimisho**

**Ndugu washiriki, Mabibi na Mabwana,**

kwa mara nyingine tena natoa shukrani zangu za dhati kwa waandaaji wa mkutano huu kwa juhudi zao katika kuleta pamoja wadau kujadili juu ya mikakati ya ushirikiano na mafanikio, ili kuwa na uwezo wa kutatua changamoto na kufanya biashara katika mazingira bora na yenye ufanisi, lakini muhimu zaidi kujiweka katika nafasi ya kukidhi matarajio ya wananchi.

Kwa kujenga nguvu na ushirikiano wetu na kulingana na mafanikio yatakayopatikana kutokana na malengo tuliyojiwekea, kwa juhudi za pamoja kati ya sekta binafsi na sekta yaumma, nina uhakika Tanzania itakuwa bora zaidi katika maendeleo ya biashara na utekelezaji wa mipango tuliyojiwekea.

Niwashukuru ninyi washiriki  wote na wadau wa maendeleo, na nafahamu tunajenga nyumba moja hivyo si busara kugombea fito, wote tushirikiane katika kutatua changamoto ili kuleta ufanisi wa mikutano hii ya mabaraza.

Mwisho, ninapenda kuutakia mkutano huu mafanikio mema kwa kuweza kufanya mjadala wenye Afya, staha, kuelewana, kuvumiliana na kuheshimiana kwa namna na njia bora zaidi.

Kwa maneno haya machache, Sasa natangaza rasmi kuwa Mkutano wa Baraza la Biashara la Mkoa wa Kigoma tarehe 24.8.2018 umefunguliwa rasmi.

***Asanteni kwa kunisikiliza***